# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

**Kikao cha Tisa – Tarehe 8 Novemba, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Reuben Kwagilwa.

Na. 134

### Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mabanda

**MHE. KWAGILA R. NHAMANILO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Mabanda – Handeni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Mabanda iliyopo Halmashauri ya Mji wa Handeni ni miongoni mwa Kata za kimkakati ambazo zimewekwa katika mpango wa kujengewa kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kata hii imeingizwa kwenye orodha ya vituo vya afya vya kimkakati 214 vitakavyojengwa katika kila Jimbo ambapo inatarajiwa kuanza ujenzi katika mwaka wa fedha 2024/2025, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Reuben.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maswali ambayo nimekuwa nikiyauliza hapa Bungeni siku zilizopita, Serikali ilielekeza kuanza kwa mchakato wa kuipandisha hadhi Zahanati ya Hedi - Kwamagome ili kuwa kituo cha afya.

Je, mchakato huo utakamilika lini ili sasa zahanati hii ya Hedi kiwe kituo kikubwa cha afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ni kweli Mheshimiwa Reuben Kwagilwa amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na maombi ya Halmashauri ya Mji wa Handeni kupandisha hadhi ya Zahanati ya Kwa Hedi - Kwamagome kuwa kituo cha afya. Naomba nimhakikishie kwamba tayari tumeshatuma wataalamu na taarifa imeshaletwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, zahanati ile inakidhi vigezo vya kupanda hadhi kuwa kituo cha afya, kilichobaki sasa tunaandaa utaratibu wa kupata fedha kwa ajili kwenda kuanza ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo hicho cha afya kitapandishwa hadhi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Kata ya Muhinda katika Jimbo la Buhigwe ni miongoni mwa kata ambazo zina sifa na vigezo vya kujengewa kituo cha kata.

Je, Kata ya Muhinda ni miongoni mwa kata mojawapo ambazo zitajengewa kituo cha afya kama ulivyozungumza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Kata ya Muhinda katika Jimbo la Buhigwe ambalo linawakilishwa na Mheshimiwa Kavejuru, ni moja ya kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amefuatilia mara kadhaa na tayari Serikali imeshaweka kwenye orodha ya kata za kimkakati ambazo zitapelekewa fedha ndani ya mwaka huu wa fedha katika mpango wa kituo cha afya kila jimbo, kata hiyo imeingizwa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kavejuru kwamba tayari fedha inaandaliwa na tutahakikisha kwamba tunapeleka fedha hiyo kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia jengo la zahanati lililojengwa katika Kata ya Mkoma, Wilaya ya Rorya kwa nguvu za wananchi mpaka kufikia hatua ya kupaua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati ambayo imejengwa katika Kata ya Mkoma katika

Jimbo la Rorya, ni kweli, kwanza nichue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete kwa namna ambavyo amefuatilia kuhusiana na jambo hili, pia niwapongeze sana wananchi wa kijiji hiki kwa kutoa nguvu zao na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua jitihada za wananchi na itaingiza kwenye mpango wa kuweka fedha mapato ya ndani au Serikali Kuu kwa ajili ya kuunga mkono nguvu za wananchi na kukamilisha zahanati hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Twaha.

**MHE. TWAHA A. MPEMBWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Kibiti tuna kituo cha afya cha muda mrefu na tunaishukuru sana Serikali kwa maboresho yanayoendelea kufanyika katika eneo hilo, je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa maabara katika kituo hiki cha afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Kituo cha Afya cha Kibiti ni kituo cha afya kikongwe na kinahudumia wananchi wengi katika Kata ya Kibiti na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge wa Jimbo la Kibiti, Mheshimiwa Twaha Mpembwene amefuatilia mara kadhaa. Naomba nimhakikishie Mbunge na wananchi wa Jimbo la Kibiti kwamba Serikali hii sikivu ya Dkt. Samia Suluhu Hassan itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa maabara hizo pia na ukarabati wa majengo hayo ambayo tayari ni chakavu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Felista Njau.

Na. 135

**Ujenzi wa Barabara ya Getifonga – Mabogini hadi Kahe – Moshi**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza: -

Je, lini Barabara ya Getifonga – Mabogini hadi Kahe itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya usanifu wa Barabara ya Getifonga – Mabogini hadi Kahe, urefu wa kilometa 31.25 ambapo mpango uliopo ni kuanza na ujenzi wa kilometa 12.0 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi bilioni 15.9. Juhudi za kupata fedha kwa ajili ya ujenzi huo zinaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia fedha za Mradi wa *RISE* kwa ajili ya kuondoa vikwazo, shilingi milioni 780 zilitengwa katika mwaka 2023/2024 ili kufanya maboresho ya kilometa 1.2 iwe tayari kupokea matabaka ya lami. Kwa sasa kazi hii inaendelea na imefikia 42% ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka 2024/2025, Serikali kupitia fedha za mafuta (tozo) imetenga shilingi milioni 775 kwa ajili kujenga kwa kiwango cha lami mita 800 ambapo kwa sasa kazi hizi ziko katika hatua ya ununuzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara inayotoka Miembeni – Dampo ambayo iko Moshi Vijijini, Kata ya Babogini,

wananchi wanatoa takataka kupitisha katikati ya mashamba ya miwa badala ya kupitisha barabarani kwa sababu barabara ni mbovu.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii?

Swali la pili, kuna barabara ya Rau – Wami – Mrawi inayoelekea *Mnambe Water Falls* ambako kuna kivutio cha watalii, barabara hii ikijengwa itavutia watalii na kuongeza Pato la Taifa na pato la mtu mmoja mmoja katika Jimbo la Moshi Vijijini. Je, ni lini barabara hii itajengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na maswali yake yote mawili naomba niyajibu kwa pamoja kuwa barabara hizi alizozitaja za Miembeni – Dampo na Barabara ya Rau – Wami, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya jitihada kubwa sana ya kuongeza bajeti katika ujenzi wa miundombinu ya barabara zetu hizi za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimfahamishe katika Mkoa wa Kilimanjaro pekee katika kipindi cha miaka mitatu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya uwekezaji wa jumla ya shilingi bilioni 153 kwa ajili ya kuhakikisha anaboresha miundombinu ya barabara zetu hizi za Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya hii ya Moshi Vijijini katika mwaka wa fedha 2024/2025 zimetengwa shilingi bilioni 8.3 kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombinu ya barabara. Pia kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri imetengwa shilingi milioni mbili katika mwaka huu wa bajeti kwa ajili ya kuhakikisha

inazifikia barabara katika Wilaya hii ya Moshi Vijijini, kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara inatekelezwa.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa dhamira ya Serikali ni kufikia barabara hizi, kuhakikisha kwamba zinajengwa, zinakuwa katika hali nzuri na zinaweza kuwanufaisha wananchi wa Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitambue kwamba Mbunge wa Jimbo, Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, naye amekuwa akisemea sana, amekuwa akipaza sauti, kwa kweli mmekuwa mkishirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba wananchi wa Moshi Vijijini wanapata barabara zilizo nzuri. Hiyo ndiyo dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha inawapelekea Watanzania barabara nzuri kwa ajili ya kuimarisha uchumi na kuhakikisha wanapata huduma nzuri za kijamii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante.

Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Bahati Ndingo.

Na. 136

**Ujenzi wa Mitaro Barabara za Vijijini - Mbarali**

**MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha barabara za vijijini ndani ya Wilaya ya Mbarali zinajengewa mitaro ili kuzuia uharibifu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mifereji ya maji ya mvua kwenye barabara zikiwemo za Wilaya ya Mbarali ambapo katika mwaka 2019/2020 mifereji ilijengwa katika

Barabara za Rujewa Mjini ambazo ni *NMB*, Mbarali – Mferejini (mita 180) kwa shilingi 9,000,000, CCM Wilaya – Rujewa (mita 280) kwa shilingi 14,000,000, Kenny – Mferejini (mita 340) kwa shilingi 17,000,000, Amini – Posta (mita 200) kwa shilingi 10,000,000. Aidha, Barabara za Igawa Mjini ambazo ni Oleneno – Shule ya Msingi Igawa (mita 200) kwa shilingi 10,000,000, Mlidi – Minzi (mita 150) kwa shilingi 7,500,000 na Pangamawe – Tankini (mita 250) kwa shilingi milioni 12.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 *TARURA* Wilaya ya Mbarali inatarajia kujenga mifejeji yenye urefu wa mita 1,000 kwa gharama ya shilingi 65,000,000 kwenye barabara ya Komba – Machicho iliyopo Igawa inayojengwa kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bahati.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri, naomba niongeze maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Igalako – Mwatenga – Mapala na Barabara ya Ipwani – Limsemi ziko katika hali mbaya kutokana na mvua zilizopita. Ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha mnakwendwa kututengenezea barabara hizo kabla ya msimu wa mvua unaokuja?

Swali langu la pili, kutokana na mvua kubwa zilizopita tumekuwa na madaraja mengi ambayo hayapitiki, ni lini sasa mtaanza ujenzi wa Daraja la Mambi na Daraja la Mloo, Wilayani Mbarali? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli anafanya kazi nzuri sana ya uwakilishi kwenye Jimbo lake la Mbarali. Naomba nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni

kuhakikisha inajenga, inaendeleza, inafanya ukarabati wa barabara zetu hizi za Wilaya ambazo zina umuhimu mkubwa sana kiuchumi na kijamii kwa wananchi, ihakikishe kwamba inazijenga hizi barabara ili ziweze kuwanufaisha wananchi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba Serikali ya Awamu ya Sita itazifikia barabara hizi ulizozitaja, lakini itafikia madaraja haya uliyoyataja na kuhakikisha yanajengwa, yanakuwa kwenye hali nzuri ili wananchi waweze kuzitumia barabara na madaraja haya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin, Mheshimiwa Zaytun ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, barabara ya kutoka Boma la Ng'ombe – Masisiwe – Idegenda iliharibiwa na mvua na haipitiki mpaka sasa; je, Serikali ina neno gani la matumaini kwa wananchi wa maeneo hayo kwa sababu mawasiliano hayakurudi tangu ilivyoharibiwa na mvua? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Justin Nyamoga kwa kuendelea kuwapambania wananchi wake kuhakikisha wanapata miundombinu bora ya barabara katika jimbo lake. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kweli amekuwa akipaza sauti kuhusiana na barabara hii na nimhakikishie kwamba Serikali itaifikia barabara hii ili iweze kuhakikisha mawasiliano yanapatikana, iweze kuwanufaisha wananchi wake kiuchumi na kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zaytun, Mheshimiwa Kakoso ajiandae.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Wilaya ya Meru inalisha karibu 60% ya wananchi wa Arusha, lakini

barabara ambazo zinasafirisha mazao haya ni mbovu sana; je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati barabara hizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kila mwaka Serikali inatenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha na inafanya ukarabati wa miundombinu ya barabara zetu hizi za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itafika katika eneo hili la Meru kuhakikisha inaboresha miundombinu hii ya barabara ili iweze kuwanufaisha wananchi na hasa kutokana na umuhimu wa barabara hii kiuchumi kwenye eneo la kilimo kama alivyoainisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Kanyasu ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kapanga – Bujombe hadi Kalya inayounganisha Mkoa wa Kigoma, Wilaya ya Uvinza na Wilaya ya Tanganyika iliahidiwa na Serikali kutolewa shilingi bilioni 1.5; je, ni lini fedha hizo zitapelekwa kwenye hiyo barabara ili iweze kuwasaidia wananchi hao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Kakoso kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi wa wananchi wake na naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba mara baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu, naomba mimi na

yeye tukae na tuzungumze ili tuweze kufuatilia utekelezaji wa ahadi hii ya shilingi bilioni 1.5 kwa maslahi mapana ya wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, jiandae Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, siku tatu zilizopita Mji wa Geita ulikumbwa na mafuriko kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha na tatizo linajulikana kwamba kuna mitaro miwili mikubwa ambayo inatakiwa kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mpango gani wa dharura ambao Serikali inao ili kuweza kuwaokoa wananchi wa Geita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi wa wananchi wake. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi na yeye tayari tulishazungumza kuhusiana na changamoto wanayoipitia katika Jimbo la Geita Mjini na hasa katika changamoto hii ya mitaro inayosababisha mafuriko. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili linafanyiwa kazi ili kuleta muafaka na kuboresha mazingira ya miundombinu ya barabara katika Jimbo lake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itajenga barabara ya kuanzia Kilosa – Mkata - *Merela Junction* ili iweze kupitika kwa mwaka mzima kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Ishengoma kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kila mwaka inatenga bajeti kwa ajili ya kufanya ukarabati na ujenzi wa hizi barabara zetu za Wilaya. Kwa hiyo, hata barabara hii aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, Serikali itahakikisha inaifikia na inaifanyia ujenzi kwa kiwango cha lami ili wananchi waweze kunufaika nayo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Geoffrey Mwambe.

Na. 137

**Utekelezaji wa Miradi ya *TACTIC* – Masasi**

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa Miradi ya *TACTIC* kwenye Halmashauri ya Mji wa Masasi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *TACTIC* umegawanyika katika makundi matatu na Halmashauri ya Mji wa Masasi ipo katika kundi la tatu ambalo utekelezaji wake utaanza kwa usanifu kufanyika mwezi Novemba, 2024 kwa kipindi cha miezi nane. Baada ya usanifu, zabuni ya kumpata mkandarasi itatangazwa mwezi Julai, 2025 na baada ya kumpata mkandarasi, ujenzi utaanza mwezi Oktoba, 2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Geoffrey.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Serikali haioni kuna haja ya kuharakisha huo usanifu ili badala ya kutumia miezi nane na miezi mitatu ya mkandarasi tukatumie miezi michache zaidi ili tuweze kuanza mradi mapema?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kutekeleza ahadi za viongozi wakuu ambako Masasi tuliahidiwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2014ujenzi wa kilometa 2.7 za lami ndani ya Mji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya katika jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba ndani ya wiki mbili tayari *consultant* atafika kwa ajili ya kuanza kazi hii ya usanifu wa kina. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya miezi hii nane japokuwa yeye anasema ni miezi mingi, lakini kwa mujibu wa taratibu baada ya miezi nane kazi hii ya usanifu itakuwa imekamilika, atatafutwa mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge huu ndiyo utaratibu na utazingatiwa na cha muhimu ni kuhakikisha wakati wa utekelezaji wa mradi atakapopatikana mkandarasi aweze kukamilisha utekelezaji wa mradi ndani ya muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mradi huu wa *TACTIC* tayari kuna *component* moja muhimu ya barabara ya lami. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za viongozi wakuu ni kipaumbele namba moja katika

mipango na katika utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami kama vile ilivyoahidiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa miji 45 ambayo ilikuwa ijengwe ya *TACTIC,* Makambako ni mojawapo ambako tunatakiwa tujengewe soko, stendi na barabara za lami pamoja na *garden*. Ni lini sasa Makambako, tupo awamu ya ngapi ili kuweza kujengewa hii ambayo tulishaahidiwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama ilivyokuwa imepangwa kwenye ratiba ni kweli miradi hii ya *TACTIC* imegawanywa kwa makundi. Kuna kundi la kwanza, kundi la pili na kundi la tatu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa mujibu wa ratiba iliyokuwa imepangwa na yeye Makambako watakuja kutekelezewa mradi huu wa *TACTIC* ili miradi aliyoiainisha iweze kutekelezwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Mbinga ni moja ya halmashauri zile 45 ambazo zinatakiwa zijengewe miradi ya *TACTIC*. Katika miradi hiyo kuna ujenzi wa barabara, ujenzi wa soko na ujenzi wa stendi mpya. Ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba mradi huo unatekelezwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya. Ninaomba nimhakikishie kwamba miradi hii inayotekelezwa katika miji 45, miradi ya *TACTIC* ipo inatekelezwa kwa mujibu wa ratiba. Nimhakikishie mpaka muda huu ratiba bado inaendelea kuzingatiwa na kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa sababu fedha ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba awataarifu wananchi wake wa Mbinga wakae mkao wa kupokea mradi huu muhimu ambao utaenda kujenga barabara, utaenda kujenga soko na stendi kama alivyoainisha Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Kwa kuwa Mji wa Njombe na wenyewe upo kwenye mradi huo, lakini ni kundi la pili, ni lini ujenzi wa miradi ya lami *TACTIC* kundi la pili inaanza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi na nimhakikishie kwamba katika mwaka huu wa bajeti mradi huu utaanza kutekelezwa katika Jimbo lake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, Halmashauri ya Mji Nanyamba ni miongoni mwa halmashauri ambazo zinatekeleza miradi ya *TACTIC* na kuna ujenzi wa soko, stendi na barabara; je, ni lini utekelezaji huu utaanza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi kwenye Jimbo lake. Nimhakikishie kwamba taratibu za utekelezaji wa miradi hii ya *TACTIC* unaendelea kwa kuzingatia kundi husika na nimhakikishie kwamba wao wapo kwenye kundi la tatu ambapo mchakato unaoendelea sasa hivi ni mchakato wa kupata *consultant* kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina ili inapofika mwakani mwezi wa saba utekelezaji wa mradi uweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wananchi wake wataweza kupata manufaa makubwa sana ya mradi huu kwa ujenzi wa soko, stendi pamoja na lami. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ukomavu wako na ubora wako.

Tunakwenda Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Neema Lugangira kwa niaba yake Mheshimiwa Mafuwe.

Na. 138

**Kupitia Upya Mkataba wa Umeme wa *REA***

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE K.n.y. MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kupitia upya Mkataba wa *REA* ili kuifanya *REA* iwe na jukumu la kufikisha umeme kwenye vituo vya huduma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kupeleka umeme vijijini ambapo hadi kufikia mwezi Oktoba, 2024 takribani 99% ya vijiji vyote vimefikiwa na nishati ya umeme. Katika utekelezaji wa miradi hiyo, vipaumbele hutolewa katika taasisi zinazotoa huduma kwa jamii zikiwemo shule, vituo vya afya, zahanati, pampu za maji na taasisi za dini ili kuboresha utolewaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kufikia mwezi Septemba, 2024 taasisi za kijamii zilizopatiwa umeme kupitia *REA*, taasisi za elimu ni 12,905, taasisi za afya ni 6,768, pampu za maji ni 5,872, nyumba za ibada ni 8,822 na maeneo ya biashara ni 29,294. Serikali itaendelea kuisimamia *REA* ili kuhakikisha inatoa kipaumbile kwenye upelekaji wa umeme kwenye taasisi za umma pale inapokuwa imekamilisha miradi ya usambazaji wa umeme vijijini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa Neema ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, sasa hivi bei au gharama ya kuunganisha umeme nyumba ambayo tayari ina umeme kwa maana ya *extension* na bei ya gharama ya nyumba mpya ambayo haijawahi kuwa na umeme inafanana.

Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kutenganisha bei hii hasa kwa nyumba ile ambayo tayari ina umeme ili iwe nafuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tunaishukuru sana Serikali imetuletea miradi zaidi ya minne ya umeme katika Jimbo la Hai, lakini bado vipo vitongoji ambavyo havijafikiwa na umeme. Kata ya Weruweru, Kata ya Mnadani, Kata ya Maili Sita, Kata ya Mnadani maeneo ya Maili Sita, pia Muungano, Boma Ng'ombe na maeneo mengine ambayo vitongoji vile havijafikiwa

na umeme. Je, lini sasa Serikali itapeleka umeme kwenye vitongoji vilivyobaki katika Jimbo la Hai? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuhusiana na gharama za kuunganisha umeme kwenye nyumba mpya na gharama za kuunganisha umeme kwenye nyumba ambayo tayari ilikuwa ina umeme na labda mita imeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kufanya *connection* kwenye nyumba ni zile zile. Gharama ya mita, gharama ya waya na *labour charge* kwa nyumba ambayo inabadilishwa na nyumba mpya gharama hazitofautiani. Kwa hiyo, gharama hizi zinakuwa *calculated* kulingana na mita, waya, pamoja na *labour* labda kama kwa maeneo ya mjini kunahitajika nguzo ndiyo pale kwa nguzo moja huwa tuna-*charge* shilingi 518,000 na ukiwekewa nguzo mbili tuna-*charge* shilingi 696,000. Hivyo, gharama za msingi za kuweka *connection* kwenye nyumba ni zilezile, ni *constant* hazibadiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge tunayo miradi ya vitongoji ambayo inaendelea pamoja na kwenye Jimbo la Hai mkandarasi yupo *site* kwa ajili ya vile vitongoji 15. Pia tuna mradi mwingine wa vitongoji ambao unakuja wa vitongoji 4,000. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Hai na wenyewe watanufaika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa. Tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Rashid Kawawa.

Na. 139

**Mradi wa Urani Eneo la Mkuju - Namtumbo**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza: -

Je, ni sababu gani zinazozuia kuanza utekelezaji wa Mradi wa Urani Mkuju - Namtumbo wakati ulishapata leseni ya uchimbaji na ujenzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini *(Special Mining Licence)* ilitolewa kwa Kampuni ya *Mantra Tanzania Limited* mwaka 2013. Hata hivyo, mara baada ya leseni kutolewa, bei ya urani ilishuka kwenye soko la dunia hali iliyosababisha uendelezaji wa mradi huu kuchelewa. Kampuni ilisubiri kuimarika kwa bei ya urani ambapo kwa sasa bei yake imeimarika na kampuni iko tayari kuendeleza mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mazingira, imeelekeza ifanyike Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira *(Strategic Environmental Assessment – SEA)* ya Ikolojia ya Mikumi – *Selous Game Reserve* ambapo mradi wa Mto Mkuju unatarajia kufanyika kwa kuzingatia *SEA* ya ikolojia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kutokana na Kampuni ya *Mantra Tanzania Limited* kuwa imekamilisha maandalizi ya kuanza uchimbaji, Serikali imeshampata mkandarasi wa kufanya tathmini hiyo ya mazingira na ameshaenda *site* tangu tarehe 3 Novemba, 2024 na anatarajiwa kuikamilisha kazi hiyo kwa muda wa miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya *SEA* itakapokamilika, itawawezesha kuanza mradi huu muhimu kwa uchumi wa Taifa na kwa wananchi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kuwa mradi huu ni wa siku nyingi sana na sasa hivi gharama ya ujenzi ambayo ilishatumika ni karibu dola milioni 300 kutekeleza mradi ule, je, Serikali inaweza ikairuhusu Kampuni ile ya Mantra kuendelea wakati utaratibu wa *SEA* unaendelea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa mradi huu hapa sasa hivi bei yake imekuwa juu, wakati tuliposimamishwa ilikuwa dola ishirini kwa paundi ya urani, sasa hivi imefika dola mia kwa paundi ya urani, je, Serikali haioni umuhimu wa sasa hivi kutumia fursa hii kwa kuwa bei yake imekuwa kubwa ili tuweze kupata manufaa ya mradi huu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mbunge wa Namtumbo ndugu yangu Mheshimiwa Kawawa kwa jinsi ambavyo amekuwa akiufuatilia mradi huu wa kimkakati na wa manufaa makubwa kwa Taifa letu. Kwa swali lake la kwanza, Serikali kuruhusu mradi kuendelea wakati imeshaitisha zoezi la kufanya tathmini ya kimazingira ni jambo ambalo nadhani itabidi lisubiri, kwanza, kwa matumaini makubwa hilo zoezi la *SEA* ambalo limeanza wiki iliyopita halitochukua muda mrefu, ni miezi sita tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kwa sababu nilitembelea *site* mwezi uliopita nikaona mtambo wa majaribio waliouweka pale na mwekezaji aliniomba kwamba ingewezekana Serikali iruhusu aendelee na mradi huo wa majaribio *(pilot project)* ambayo ameanza mtambo mdogo, nilimhakikishia kwamba Serikali itafikiria na bado inaendelea kulifanyia kazi ombi hilo. Kama litajibiwa kabla ya *SEA* kukamilika basi atapata majibu yake maana Serikali haina kipingamizi na kuhakikisha kwamba mradi huu wenye tija unatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, ni kweli bei ya urani sasa hivi imepanda duniani na ni madini yenye thamani kubwa kwa sasa. Sisi kama Serikali hatuna sababu ya kuuchelewesha huu mradi zaidi ya kuhakikisha usalama wa mazingira yetu ukizingatia kwamba eneo husika lipo pembezoni au ndani ya eneo la hifadhi ambalo ni Selous pamoja na *Mwalimu Nyerere National Park. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hicho ndicho kikwazo, lakini tuna hamu kubwa ya kuona mradi huu utaendelea. Hii *SEA* itakapojibu ndani ya miezi sita ijayo, tutauona mradi huu ukianza kutekelezwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Benardeta Mushashu.

Na. 140

**Kukamilisha Ujenzi wa Jengo la Kuwatenga Walioathirika na Magonjwa ya Mlipuko**

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa jengo la kuwatenga walioathirika na magonjwa ya mlipuko Kagera?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la kuwahifadhi wahisiwa wa magonjwa ya kuambukiza lililopo katika mpaka wa Mutukula, Wilaya ya Missenyi, Mkoa wa Kagera ambalo limegharimu kiasi cha shilingi milioni 140. Kwa sasa jengo hilo limekamilika na limewekewa huduma za maji, umeme, kuwekewa vitanda na tayari limeanza kutumika kuwahifadhi wanaohisiwa kuwa na magonjwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 kiasi cha shilingi milioni 80 kimetengwa kwa ajili ya maboresho ya sehemu ya nje ya jengo hilo ikiwamo kuweka sehemu yenye kivuli *(lounge)* kwa ajili ya wasafiri, pamoja na uwekaji wa viyoyozi na samani nyingine kwa ajili ya utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benardeta

**MHE. BENARDETA K. MASHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaishukuru Serikali kwa kutujengea hicho kituo kidogo pale Mutukula cha kuwatenga wanaohisiwa kwamba wana magonjwa ya mlipuko kule Mtukula, Wilayani Missenyi.

Je, ni lini sasa Serikali itaona umuhimu na kujenga vituo vya namna hivyo kwenye mipaka pale Mulongo – Kyerwa, Rusumo pamoja na Kabanga kule Ngara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Kagera umepakana na nchi jirani kadhaa, kwa hiyo, ni rahisi kupata haya magonjwa ya mlipuko kama *Marburg* na Ebola, je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kutujengea hospitali kubwa ya magonjwa ya kuambukiza *(infectious disease hospital)* kusudi hao wanaotambulika kwenye hivyo vituo *(isolation centers)* kama ya Mutukula wapate mahali ambapo wataenda kupata matibabu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge sio tu kwa sababu ya swali lake hili, lakini kwa sababu ya kazi ambayo tumekuwa tukifanya pamoja kwa miaka yote hii minne kwa ajili ya Wana-Kagera, lakini kwa ajili ya wanawake wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ni lini tutaweza kujenga maeneo kama hayo kwenye maeneo mengine. Kwa kweli fedha zinaendelea kutafutwa sio tu kwenye maeneo ya Mkoa wa Kagera, lakini ni mipakani kote Kigoma, upande wa Kusini na kila mahali kuhakikisha tupo vizuri inapofika kuna magonjwa ya mlipuko kwa majirani zetu ili tuweze kujikinga pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kujenga hospitali kubwa, moja, kwanza Mkoa wa Kagera una hospitali moja kubwa ya Mkoa na Hospitali hiyo kubwa inaendelea kupanuliwa na kuwa kubwa zaidi na kuwekewa mambo mbalimbali kwa sababu kikubwa sio kujenga hospitali ya magonjwa ya kuambukiza, kikubwa ni kuhakikisha hayo magonjwa hayaingii Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuwahakikishia jinsi uhitaji unapoonekana tutaenda kufanya hayo, lakini nataka kukuhakikishia hospitali yenu ya mkoa itaenda kupanuliwa na kuwa kubwa sana na kuwa na vitengo vya magonjwa mbalimbali yanayosibu watu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Kisangi.

Na. 141

**Taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa**

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa ili kupunguza vifo vinavyotokana na mabadiliko ya hali ya hewa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* imeendelea kuwezesha miundombinu ya ukusanyaji, uchakataji na ufungashaji wa taarifa za hali ya hewa hapa nchini. *TMA* imeendelea kufanya usambazaji wa taarifa hizo za hali ya hewa kwa umma kupitia vyombo vya habari mbalimbali na kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri mimi kwanza naipongeza Mamlaka ya Hali ya Hewa inafanya kazi nzuri sana ya kutoa tahadhari ya hali ya hewa ya nchi yetu na tahadhari ambazo ni za ukweli kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa taarifa za hali ya hewa zinatolewa mapema sana, lakini Serikali haichukui hatua za mapema matokeo yake kunatokea madhara makubwa sana kama vile inaponyesha mvua kubwa katika maeneo mbalimbali. Je, mamlaka zinazohusika zina mpango gani sasa wa kuhakikisha wanafanyia kazi taarifa za hali ya hewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa tumeshuhudia kunyesha kwa mvua kubwa katika maeneo na kusababisha mafuriko kama vile ya Rufiji, Kibiti, Kilwa, Lindi na Arusha - King'ori kulitokea mvua kubwa, madaraja yakavunjika mpaka gari la wanafunzi likaingia kwenye daraja.

Je, Serikali imejipanga vipi sasa kutoa taarifa pale inapotokea mvua inanyesha angalau kusimamisha masomo kwa wanafunzi wa shule za msingi na *nursery school*? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutoa pongezi

kwa Mamlaka yetu ya Hali ya Hewa kwa kazi kubwa ambayo wanafanya na hii ni kutokana na uwekezaji mkubwa sana ambao Serikali imefanya katika kuiwezesha mamlaka hii itoe taarifa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, amezungumza kuhusu kufanyia kazi, Mamlaka ya Hali ya Hewa ina jukumu kubwa la kuangaza, kukusanya, kuchakata pamoja na kuhifadhi na kusambaza taarifa za hali ya hewa na mara baada ya kukamilisha jukumu hilo la kwanza, jukumu la pili ambalo linafanyika sasa ni namna gani taarifa hizo zinakwenda kuwafikia wananchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri tunayo sheria ya mwaka 2006 ambayo ni Sheria yetu ya *TMA* inaipa mamlaka kufanya kazi hiyo, lakini pia tuna Sheria ya Maafa Namba 6 ya mwaka 2022 ambayo kimsingi inatoa nafasi kwa Kamati zetu za Maafa mbalimbali nchi nzima. Mara baada ya kupokea taarifa za *TMA*, kuhakikisha kwamba zinasambazwa na kufikishwa katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Serikali kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali imeendelea kutoa elimu mbalimbali kwa wananchi kupitia vyombo vya habari, kuimarisha mifumo yetu ya tahadhari pamoja na kujenga uwezo wa watendaji ili kuhakikisha kwamba taarifa zinakuwa sahihi, lakini pia zinafika kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru pia kwa swali lake la pili juu ya ushauri alioutoa kwamba pengine inapotolewa taarifa hizo za hali ya hewa pengine kutakuwa labda na kimbunga na kadhalika, ni vyema shule zikafungwa. Ushauri huu ni mzuri na sisi kama Serikali tumeupokea, tutaenda kuuchakata na kuufanyia kazi hatua kwa hatua. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakar Hamad.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru, ni kweli kwamba Mamlaka yetu ya Hali ya Hewa

inafanya kazi nzuri hivi sasa kutokana na uwekezaji mkubwa ambao Mheshimiwa Rais ameuwekeza, lakini kumekuwa na changamoto kwa wadau na taasisi mbalimbali zinazotumia taarifa hizi, kuchelewesha malipo kwa mamlaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na taasisi hizi ambazo zinachelewesha malipo baada ya kutumia taarifa za hali ya hewa ili taarifa zetu za hali ya hewa ziendelee kuwa endelevu na bora zaidi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Bakar kwa swali lake la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia nafasi hii kuomba taasisi mbalimbali ambazo kimsingi ni wanufaika wa taasisi hii au taarifa za taasisi hii ili waweze kulipa ndani ya muda kwa ajili ya kusaidia mamlaka yetu ipate fedha na kuongeza uwezo zaidi, iweze kutengeneza au kuandaa taarifa zingine sahihi zaidi kuliko pengine livyokuwa hapo mwanzoni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ulinzi. Mheshimiwa Asia.

Na. 142

**Ajira kwa Vijana wa JKT Walioshiriki katika Ujenzi katika Maeneo Mbalimbali**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuwaajiri vijana wa JKT walioshiriki ujenzi wa ukuta wa Mererani, Ikulu na maeneo mengine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa mwaka 1963 kwa lengo la kutoa mafunzo ya uzalendo, ulinzi na malezi kwa vijana wa Kitanzania. Mafunzo hayo, yanalenga kuwafundisha umoja na mshikamano, ukakamavu na kuwa tayari kulitumikia Taifa lao wakati wote. Katika mafunzo hayo, vijana hufundishwa pia stadi mbalimbali za kazi na maisha. Lengo ni kuwawezesha vijana hao kuwa na uwezo wa kujitegemea baada ya mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania huandikisha askari wapya kwa mujibu wa sheria, kanuni na maelekezo yanayotolewa mara kwa mara, kama ilivyofafanuliwa katika kanuni ya tano ya Kanuni za Majeshi ya Ulinzi, Juzuu ya Kwanza ya Utawala. Hivyo, vijana wote wanaojiunga na JKT huandikishwa kwa kufuata utaratibu. Hapa wanaojiunga na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, wanaoandikishwa, huandikishwa kwa kufuata utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2019 hadi 2022, jumla vijana 5,744 waliokuwa na sifa ikiwa ni pamoja na wale walioshiriki katika ujenzi wa ukuta wa Mererani na Ikulu waliandikishwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kufuata utaratibu niliouelezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza ninauliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali yetu kwa kuendelea kuwajenga vijana katika misingi ya uzalendo, lakini katika misingi ya stadi za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, kwa kuwa Serikali iliona kazi maalumu na kubwa ambayo imefanywa na vijana waliofanya kazi hiyo ya *operation,* waliojenga Ikulu pamoja na ukuta wa Mererani.

Je, Serikali haioni haja ya kuwachukua pia vijana waliojenga Chuo cha Mzumbe, Bwawa la Mwalimu Nyerere, nyumba za Ukonga pamoja na Msomela kwa sababu kazi za *operation* hazitokei kila mara, ni kazi ambazo zinatokea mara chache. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuwachukua na vijana hao waliojenga maeneo mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Serikali haioni kuwa kwa kuwa JWTZ itakuwa ina nafasi labda zisizokidhi vijana wote. Serikali haioni haja sasa kuungana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ili kuwa na ile *database* ya vijana ambao wamefanya kazi maalumu, wakaweza kuwekwa kwenye majeshi mengine? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, swali la kwanza ambalo ameuliza, kuwachukua vijana wengine ambao wameshiriki katika *operation* mbalimbali alizozitaja, utaratibu wa kuwachukua vijana ni kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninafurahi na ninamshukuru kwamba katika swali lake la pili, ameeleza wazi nafasi za kuandikisha vijana jeshini ni chache. Kwa hiyo, tunawachukua vijana kulingana na mahitaji ya wakati huo, kulingana na taaluma walizonazo na vijana wote wanaopenda JKT hushiriki katika *operation* mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawashukuru sana vijana wetu kwa moyo huo wa kujitolea na kufanya kazi hizi wanazokuwa wamepangiwa kwa umahili wa hali ya juu. Kwa hiyo, kadiri nafasi zinavyopatikana na kadiri mahitaji ya wakati huo yalivyo vijana mbalimbali huchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwa na *database*, *database* ipo na tunashirikiana na vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama katika kuainisha vijana kuja kwetu. Kuainisha vijana ambao wana sifa kulingana na mahitaji yao. Kwa hiyo, tunafanya kazi pamoja na *database* ipo, lakini ikumbukwe tu kwamba Bunge hili lilitoa pia uhitaji au kigezo hicho. Kwa hiyo, pengine ni kulishauri Bunge likaangalia upya kigezo hicho ambacho kiliondolewa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Juma Othman Hija, kwa niaba.

Na. 143

**Hitaji la Makazi ya Polisi Kituo cha Mkokotoni – Tumbatu**

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS K.n.y. MHE. JUMA OTHMAN HIJA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la makazi ya askari Kituo cha Polisi Mkokotoni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeshatenga eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 2,500 ambalo litatumika kujengwa maghorofa sita yatakayoishi jumla ya familia 24 za askari polisi. Fedha kwa ajili ya ujenzi huo zinatarajiwa kuanza kutengwa kwenye bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tamima.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba Serikali sasa kwa vile tayari imesema itatenga fedha iwaone na iwasaidie kwa

dharura kwa kipindi hiki cha mpito wale askari ambao wanaishi mbali na kituo hicho. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, tumeupokea ushauri na ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Jeshi la Polisi tunafanya tathmini kuhakikisha majengo yote ambayo ni chakavu, yanakarabatiwa, lakini tunajenga majengo mapya, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutahakikisha askari wetu wanakaa katika maeneo ambayo yako salama kwa ajili ya kulinda raia na mali zao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Maswa ni wilaya kongwe kabisa katika Mkoa wa Simiyu, lakini haina Kituo cha Polisi, je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Maswa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha tunajenga Vituo vya Polisi vya Kata na Ofisi za Wilaya nchi nzima pamoja na shehia kwa upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya ya Maswa ambayo haina Kituo cha Polisi pia tutaitengea fedha na kujenga Kituo cha Polisi kwa ajili ya usalama wa wananchi wa Maswa na vitongoji vyake, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itajenga nyumba za askari polisi katika Mkoa wa Simiyu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninajibu swali la Mheshimiwa Minza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua askari wetu wengi hawana nyumba za kuishi, lakini ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tunafanya tathmini nchi nzima kuhakikisha kwamba upungufu wa nyumba uko kiasi gani ili tuweze kutenga katika bajeti zetu mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil, na Mheshimiwa Butondo, ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Masasi imeendelea kukua, lakini nyumba za polisi zilizopo zimechakaa na ni za muda mrefu. Je, Serikali haioni haja ya kujenga nyumba mpya kwa ajili ya askari polisi wa Wilaya ya Masasi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninajibu swali la Mheshimiwa Cecil Mwambe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, timu yetu ya wataalamu inapita nchi nzima kupitia nyumba zetu za askari polisi na kuona jinsi ambavyo zimechakaa ili sasa tupange, tujenge awamu kwa awamu kwa sababu hatuwezi kujenga zote kwa mara moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru, wananchi wa Jimbo la Kishapu bado wanahangaika kuhusiana na kituo cha afya cha wilaya. Tumejenga kwa kutumia nguvu za wananchi, Mfuko wa Jimbo pamoja na Mgodi wa *Williamson Diamond Limited*. Mradi huu unahitaji jumla ya shilingi 175 kwa ajili ya kukamilisha, Mheshimiwa Naibu Waziri aliyepita kipindi kilichopita, alifika katika kituo hicho na akaahidi mwaka huu wa fedha watakamilisha kituo hicho cha wilaya...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itakwenda kukamilisha mradi huu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninajibu swali la Mheshimiwa Butondo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Serikali imeahidi kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha wa 2024/2025 kuwa inamalizia maboma 77 na imetenga takribani shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge pia boma lake la Kishapu tutaweka kwenye mpango na kumtengea fedha ili kuweza kukamilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sigula.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Wilaya ya Nkasi haina kabisa nyumba za askari, jambo ambalo linasababisha usalama hafifu wa familia zao na utendaji hafifu wa kazi. Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza nyumba za askari polisi katika Wilaya ya Nkasi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvia Sigula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu maswali mengi ya nyongeza, Serikali inafanya tathmini kuangalia upungufu wa nyumba za askari katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo na Wilaya ya Nkasi aliyoitaja ili tuweze kutengea bajeti kwenye mpango na kutenga fedha kwa ajili ya nyumba za askari polisi kujengwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

Na. 144

**Ujenzi wa Benki – Micheweni**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka huduma ya benki ya *NMB* na *CRDB* kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Micheweni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuimarisha uchumi wa maeneo yote ya nchi ili kuweka mazingira yatakayovutia benki na taasisi za fedha kuanzisha huduma za kibenki katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki za *NMB* na *CRDB* hazina matawi kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Micheweni. Hata hivyo, wananchi wa Wilaya ya Micheweni wanapata huduma za kibenki kutoka Benki za *CRDB* na *NMB* kupitia mawakala wa benki, ambapo hadi kufikia Oktoba, 2024 kulikuwa na jumla ya mawakala wanne wa Benki ya *CRDB* na mawakala 14 wa Benki

ya *NMB* wanaotoa huduma za kibenki katika Wilaya ya Micheweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kufungua matawi ya benki hufanywa na benki yenyewe. Kabla ya benki kufanya uamuzi wa kufungua tawi jipya, benki husika hufanya upembuzi yakinifu ukiwa na lengo la kuangalia kama kuna uwepo wa biashara ya kutosha ambayo italeta faida kwa benki husika. Benki zikishafanya upembuzi yakinifu katika sehemu husika huwasilisha mapendekezo yao kwa Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Benki Kuu haina kizuizi chochote katika suala la benki kufungua matawi, kama benki husika itatimiza masharti yote ya kufungua matawi kama yalivyoanishwa katika kanuni namba 31 ya Kanuni za Utoaji Leseni za Benki na Taasisi za Fedha za mwaka 2014.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kombo.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni muda gani wa mwisho ulifanyika upembuzi yakinifu kwa benki hizi katika Wilaya yetu ya Micheweni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, kuna maombi yoyote ya ufunguzi wa matawi mapya ya benki katika Wilaya yetu ya Micheweni yaliyopelekwa, ukizingatia kazi kubwa ya maeneo ya uwekezaji inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi katika Wilaya yetu ya Micheweni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Issa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu ninaomba kumpongeza sana yeye pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Micheweni kwa namna wanavyopambana ili huduma za kibenki kupatikana ndani ya Wilaya ya Micheweni hasa makao makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uridhie nijibu maswali yote mawili kwa pamoja kuwa hadi sasa bado Serikali haijapokea maombi kwa Benki za *NMB* na *CRDB* kufungua tawi jipya pale makao makuu ya Wilaya ya Micheweni, lakini kutokana na uwekezaji ambao umewekwa na Serikali ya Awamu ya Nane, inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi katika Wilaya ya Micheweni, mfano, kama ujenzi wa bandari mpya ya kisasa na viwanda mbalimbali na ni eneo husika la uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba benki zetu za *NMB* na *CRDB* na benki nyingine, waende kuangalia fursa hii na wafanye upembuzi yakinifu kwa ajili ya kufungua tawi katika makao makuu ya Wilaya ya Micheweni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Amandus Chinguile.

Na. 145

**Uhakiki wa Wastaafu kwenye Halmashauri au Kata badala ya Mkoani**

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa wastaafu kuhakikiwa kwenye halmashauri au kata badala ya utaratibu wa sasa wa kuhakikiwa mkoani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakiki wa wastaafu wanaolipwa na Hazina umekuwa ukifanyika katika ngazi ya halmashauri. Hata hivyo, ili kupunguza gharama za wastaafu kwenda kujihakiki na kuwaondolea usumbufu wa kusafiri umbali mrefu ili kupata huduma ya kuhakikiwa, Serikali inatengeneza mfumo wa kidigitali utakaowawezesha wastaafu kujihakiki wenyewe kupitia simu zao za mkononi au kwa kutumia huduma za kibenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa taratibu zote wastaafu watapewa elimu ya jinsi ya kujihakiki wenyewe na watatangaziwa siku ya kuanza kujihakiki, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amandus.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali yanayoonesha namna wanavyojali wastaafu, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wastaafu ambao wanaishi vijijini na mbali sana na makao makuu ya halmashauri na afya zao wakati mwingine siyo nzuri, wakati Serikali inatengeneza mfumo mpya wa kidigitali, je, haioni haja sasa ya kuwasogezea huduma wazee hawa wastaafu ambao hali zao siyo nzuri kwa kutumia watendaji wa kata na vijiji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, ni mshahara gani hutumika katika kutengeneza *pension* hizi za wastaafu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kabla ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge ninaomba nimpongeze sana kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, kwa kufuatilia jambo hili siku hadi siku. Ni mara kadhaa tunakutana ofisini kujadili suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue swali lake la kwanza kama ni ushauri, hivyo ushauri wake umepokelewa, tunaenda kuufanyia kazi, kwa sababu Serikali imeona hilo na

ndiyo maana tukasema tunaenda kuanzisha mfumo maalumu wa kidigitali ambao utawawezesha wastaafu kujihakiki wenyewe kupitia simu zao za mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, mshahara ambao unazingatiwa wakati wa kutengeneza *pension* ni ule mshahara wa mwisho wa mtumishi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alice.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni swali la kutumia teknolojia na Mheshimiwa Waziri ameshajibu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jane.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Maboresho hayo ni lazima yaendane na nyongeza ya kima cha malipo ya pensheni. Ni lini mtawaongezea hawa wastaafu wanaolipwa na Wizara ya Fedha kiwango cha malipo kila mwezi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ongezeko la fedha ama la peshneni kwa wastaafu wetu ni suala ambalo linafuata taratibu na mchakato sasa hivi upo unaendelea nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira ataona matokeo chanya baada ya siku chache...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante! Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Jacqueline Kainja.

Na. 146

**Kuwezesha Mawasiliano ya Redio Tarafa za Wilaya ya Sikonge**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaona umuhimu wa kuwezesha mawasiliano ya redio kwa Tarafa ya Kiwele, Kata za Kitunda, Uloli, Kilumbi na Kipili – Sikonge?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania limejenga mitambo ya kurushia matangazo ya redio masafa ya *FM* katika eneo la Usungilunde Kata ya Sikonge, Wilayani Sikonge ambapo *TBC* Taifa inapatikana katika masafa ya 87.9 *MHz* na *Bongo FM* masafa ya 89.9 *MHz*. Mitambo hii inafikisha matangazo umbali wa kilometa 60 za hewani *(Air distance)* kutoka Usungilunde. Kata ya Kitunda ipo umbali wa zaidi ya kilometa 130 za hewani, Uloli, Kilumbi na Kipili zipo umbali wa zaidi ya kilometa 140 za hewani, hivyo kutokufikiwa na matangazo ya *TBC* kutokea mnara uliopo Eneo la Usungilunde Kata ya Sikonge. Serikali kupitia *TBC* imeweka maeneo haya katika utekelezaji wa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nami kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukubwa wa Wilaya ya Sikonge na Tarafa ya Kiwele kutoka Kata ya Kitunda kwenda Kipili ni umbali wa kilometa za hewani 140. Je, Serikali kutokana na Mpango wa 2025 imepanga kuweka minara mingapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Jacqueline kwa ufuatiliaji wa mawasiliano ya uhakika kwa wananchi wa eneo hili lakini pili kama mwenyewe ulivyokiri ni umbali wa kilometa 140 wataalamu wetu wataendelea kufanya *study* ya kuona ni kiasi gani tuweze kuweka minara lengo ni kuhakikisha taarifa, mawasiliano, redio ziweze kusikika katika maeneo haya ambayo umeuliza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usikivu wa Redio Tanzania katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa Jimbo la Muhambwe ni hafifu sana, kama kule Kuninama, Mukabuye na Mkarazi hali inayochangia wananchi hawa kusikiliza redio za nchi jirani hivyo kukosa taarifa muhimu za nchi yao. Je, ni lini Serikali itaboresha usikivu wa Redio Tanzania katika vijiji vya pembezoni vya Jimbo la Muhambwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Florence, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema maeneo haya ya pembezoni Redio Tanzania inasikika kwa mbali lakini tayari tupo kwenye mikakati *TBC FM* itaendelea kuchakata na kuona maeneo ya pembezoni pamoja na Muhambwe katika kijiji hiki ulichokisema tunaweza kuyafikia na kuhakikisha wananchi wanapata taarifa za ndani ya nchi kwa sababu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kazi nyingi ni vyema wananchi wakapata taarifa kwa muda sahihi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Mwanyika.

Na. 147

**Hitaji la Mnara wa Mawasiliano Kijiji cha Uliwa – Njombe**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa mnara wa mawasiliano katika Kijiji cha Uliwa - Njombe utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Kijiji cha Uliwa kipo katika Kata ya Iwungilo inayoundwa na vijiji vya Ngalanga, Iwungilo, Igoma na Uliwa, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* ilijumuisha Kata ya Iwungilo katika mradi wa mawasiliano wa awamu ya pili '*A*' *(2A)* ambapo mtoa huduma *HONORA (TIGO)* alijenga minara katika vijiji vya Iwungilo na Ngalanga inaohudumia vijiji vya Ngalanga, Iwungilo, Igoma na Uliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *UCSAF* ilifanya tathmini katika Kijiji cha Uliwa na kubaini kuwa kulingana na jiografia ya kijiji cha Uliwa ambacho kipo bondeni, minara iliyojengwa awali haifikishi mawasiliano katika kijiji hiki. Hivyo, *UCSAF* tayari imekijumuisha kijiji hiki katika orodha ya vijiji vitakavyonufaika kupitia mradi wa mawasiliano vijijini utakaotekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deodatus.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, ninashukuru kwa majibu ya Serikali na kwa kutambua kwamba kweli Uliwa wana tatizo la mawasiliano, sasa nina maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kwa sababu kijiji hiki kina mahitaji makubwa yanayotambulika, ni lini sasa Serikali itaanza

ujenzi? Kwa sababu nimeuliza hili swali zaidi ya mara tatu hapa na nikahakikishiwa itaingia kwenye Mradi wa Minara 758 lini Serikali itanza ujenzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili nilitaka kujua kama inaonekana kuingiza kwenye bajeti ya kawaida ya Serikali ambayo ndiyo imesemwa hapa mnara unachuka muda mrefu kujengwa ni kwa nini sasa tusihamishe huu mnara tukauhamishia kwenye Mradi wa Minara 748 kwa sababu sisi tuna mnara moja tu na tunaweza tukafanya *switching*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusi lini tuaanza ujenzi, ni jana tu Mheshimiwa Mbunge aliweza kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri wetu Mheshimiwa Jerry Silaa na akaunganishwa na Mtendaji Mkuu wa *UCSAF* Kaka yangu *Engineer* Peter Mwasalanda na *Engineer* Mwasalanda ameshamwagiza *engineer* anayehusika na maeneo ya Nyanda za Juu Kusini na tayari anajiandaa kuelekea kwenye Kijiji hiki cha Uliwa kufanya tathmini ili tuone *population* iliyopo pale Uliwa ili wapate mawasiliano ya uhakika. Ninakupongeza sana Kaka yangu Mheshimiwa Deodatus umefuatilia kweli mara nyingi na sasa tutakuja kulifanyia kazi tumekuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *switching* ya mnara mmoja kwenda eneo lingine Mheshimiwa Mbunge ninaomba baada ya hapa tukutane tena kama ulivyoongea jana na Mheshimiwa Jerry tutawasiliana na *DG* Peter lengo ni kuhakikisha tunafanikisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Mheshimiwa Rais wetu alisaini Minara 758 lakini hata mimi kwenye Jimbo la Kalenga Vodacom walisaini katika Kata ya Masaka Kijiji cha Kaning'ombe. Kwa kuwa Vodacom wamecheleweshа kujenga mnara mpaka sasa hawaoni kufanya hivyo ni kuhujumu juhudi za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuwaletea maendeleo Wananchi wa Kalenga? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Vodacom ndio wanaowajibika kujenga mnara pale sisi kama Wizara hatutaruhusu hujuma yoyote kwa nguvu anazoziweka Mheshimiwa Rais wetu. Nikuhakikishie mnara huu utajengwa na tutausimamia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe. Mheshimiwa Sichalwe, kaa chini Mheshimiwa Magessa

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini mnara wa Msasa uliokuwa katika ile Minara 758 utaanza kujengwa kwa sababu ilisainiwa minara miwili lakini wa Msasa mpaka sasa hivi haujaanza kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Magessa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia mnara huu na kama tulivyoongea hapo nje nikuhakikishie nitasimamia utekelezaji huu wa mnara uweze kufanyika na mawasiliano ya uhakika yaweze kupatikana kwa wananchi wa eneo wako unaowakilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi Mungu akubariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Kasinde Kata ya Kapele, Kijiji cha Ntungwa Kata ya Mkomba, Kijiji cha Naming'ongo Kata ya Chitete havina mawasiliano kabisa pamoja na vijiji vingine na nimeuliza hii ni mara ya nane hapa Bungeni. Wizara mna mkakati gani wa kutusaidia mawasiliano kwenye Jimbo la Momba? Ahsante!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Nimpongeze Mheshimiwa Condester kwa swali lake. Pole sana kwa kufuatilia kwa muda mrefu lakini hakuna refu linalokosa ncha nikuhakikishie tutakuja kutekeleza. Vijiji vyote hivi ulivyovitaja tutakuja kutembelea na baada ya hapa nitamwagiza yule Mtendaji wa Nyanda za Juu Kusini aweze kufika pale Momba na lazima tuhakikishe ndani ya mwaka huu wa fedha tuweze kuona nini kinafanyika angalau katika eneo moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zidadu.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa kujenga mnara wa mawasiliano wa simu katika Kata ya Ngapa lakini mawasiliano yale ya simu hayafiki katika Kitongoji cha Ngapa *B* ama Ngapa Mtoni ambapo kuna wachimbaji wengi sana na wanakosa huduma ya mawasiliano ya simu. Je, Serikali haioni haja ya kwenda kuongeza nguvu katika ule mnara ili uweze kufikisha mawasiliano ya simu Ngapa Mtoni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la uchimbaji ni eneo muhimu sana katika uzalishaji na Pato la Taifa tupo tayari kuja kuongezea nguvu na wananchi waweze kupata mawasiliano ya uhakika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante! Tunaenda Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahawanga.

Na. 148

**Mafunzo kwa Wasindikaji Wadogo wa Vyakula Nchini**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, lini *TBS* itaweka utaratibu wa kutoa elimu kwa wajasiriamali wadogo wanaojihusisha na biashara ya kusindika vyakula?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)*, inatekeleza programu ya kutoa mafunzo kwa

wajasiriamali wadogo na wakati *(SMEs)* kwa kushirikiana na *SIDO* pamoja na wadau mbalimbali katika dhana nzima ya viwango kwa kuhimiza uzingatiaji wa viwango katika uzalishaji wa bidhaa ili kukidhi matakwa ya ubora na ushindani katika soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2023/2024, jumla ya wajasiriamali wadogo na wadau wa sekta mbalimbali 14,354 walipatiwa mafunzo ya ubora. Aidha, kupitia programu hiyo Serikali kupitia *TBS* imekuwa ikitenga takribani milioni 350 kila mwaka kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo na wakati *SMEs (Small and Medium Enterprise)*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza nini mpango wa *TBS* kuhakikisha inawasaidia wajasiriamali wadogo kupata alama ya bidhaa zao, alama za ubora za bidhaa zao kwa gharama nafuu lakini pia kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, *TBS* ina mkakati gani kuhakikisha inafungua vituo vya kutoa huduma kwa wajasiriamali wadogo hususan kwenye maeneo ambayo hayawezi kufikika kwa urahisi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi ni dhamira ya Serikali ya *TBS* kuwaimarisha hawa wajasiriamali wadogo na ndiyo maana utaona tumeweza kuwafikia zaidi ya 14,354. Sasa kwa sababu kama ilivyoelezwa huenda kutokana na ukubwa wa eneo analotoka la Dar es Salaam wajasiriamali ni wengi tutaimarisha *TBS* kwa sababu makao makuu yake yapo Dar es Salaam

kuwafikia kwenye ngazi za Wilaya ili wengi zaidi waweze kupata huduma kwa gharama nafuu, ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar, jiandae *Engineer* Samweli.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Kwa kuwa baadhi ya wafanyabiashara wanaouza bidhaa kama vile chakula vinywaji na madawa kwa ajili ya matumizi ya binadamu siyo waaminifu kwa kuendelea kuuza bidhaa ambazo zimeisha muda wake. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka ili kuweza kutoa elimu kwa wananchi hasa kule chini kuzuia kuendelea kutumia bidhaa hizo na kusababisha madhara makubwa kwa wananchi wetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Amar kwamba wapo wafanyabiashara wasiyo waaminifu ambao huweza kuuza bidhaa zilizopitwa na muda wake kwa kulijua hilo na kwa sababu Mamlaka ya Udhibiti wa Viwango ipo makao Makuu Dar es Salaam kwa mujibu wa Sheria ya Viwango, mamlaka za wilaya kwa maana ya halmashauri wataalamu wake wamekasimiwa majukumu ya ukaguzi wa bidhaa katika maduka, *pharmacies* na kadhalika ili kuwabaini watu hao na kuchukua hatua stahiki. Kweli wanapobainika hatua kali huchukuliwa ikiwa ni pamoja na uharibifu wa bidhaa hizo na kuwafikisha Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kupitia hadhira hii nihimize Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambao wamekasimiwa jukumu hili…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** …wamekasimiwa jukumu hili kulitekeleza kwa umakini ili kuondoa malalamiko kama haya, ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ya usindikaji wa chumvi na magadi ambayo yanapatikana kwa wingi Ziwa Gendabi na Balangdalalu ili wananchi wa maeneo hayo waweze kunufaika na rasilimali zinazopatikana kwenye maeneo yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua umuhimu wa Serikali kuwasaidia wasindikaji wadogo wakiwemo wa chumvi na magadi kwa kutambua umuhimu huo ndiyo maana Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanda Vidogo *(SIDO)* hutoa mafunzo ya mara kwa mara kwenye maeneo yetu mbalimbali ikiwemo Hanang ili wafanyabiashara wa namna hii waweze kupata utaalamu wa kusindika chumvi kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na Serikali,ahsante!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Abubakari Asenga.

Na. 149

**Kufufua Kiwanda cha *Mang'ula Machine Tools***

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, lini Kiwanda cha *Mang'ula Machine Tools* kitafunguliwa baada ya kufungwa kwa muda mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa katambua umuhimu wa Kiwanda cha *Mang'ula Machine Tools* katika uzalishaji wa mashine na vipuri nchini, Serikali imekusudia kukifufua Kiwanda hicho na kuwezesha kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya mitambo, kukarabati badhi ya majengo, uhakiki mali *(stocktaking)* na uthamini mali wa kiwanda *(valuation)* ambapo thamani ilibainika kuwa shilingi bilioni 9,571,000,000 kulingana na taarifa ya tarehe 21 Machi 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua itakayofuata ni kutafuta Mbia mwenye uwezo wa kifedha na teknolojia inayohitajika kwa ajili ya kufufua kiwanda hiki. Aidha, kutokana na mpango kazi inatarajiwa mwekezaji apatikane mwishoni mwa Mwezi Februari 2025, ukarabati wa majengo na usimikaji mitambo kukamilika mwezi Disemba, 2025 na hatimaye uzalishaji kuanza Januari, 2026, ahsante!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na niishukuru Serikali. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara amefanya ziara katika kiwanda hiki tunamwomba Mungu hiyo mipango ya Serikali itimie.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ama ombi langu ni moja tu wakati huu pale kuna ekari karibu 250 kumekuwa na pori kubwa na watu wahalifu wanajificha pale ndani. Je, ni upi mpango wa Serikali wakati tunasubiri uwekezaji kufanyika kwa usafi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni sahihi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge Abubakari Asenga kwamba haiwezekani eneo la kiwanda zaidi ya ekari hizo zigeuke kuwa

pori katika Mji ule wa Mang'ula. Kupitia Bunge lako Tukufu nimwelekeze Mtendaji Mkuu wa *NDC* kuchukua hatua za kufanya usafi katika eneo lile na kuimarisha ulinzi ili kuhakikisha usalama wa mali zilizopo katika Kiwanda wa Mang'ula, ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante! Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Jumbe Mlaghila.

Na. 150

**Fidia kwa Wananchi Wanaopisha Ujenzi wa Barabara – Kyela**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza:-

Je, lini wananchi wanaopisha ujenzi wa barabara ya Ibanda – *Itungi Port* wa Iponjola - *Kiwila Port* watalipwa fidia zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la uthamini wa mali za wananchi zitakazoathirika wakati wa ujenzi wa barabara ya Ibanda – *Itungi Port* na Iponjola – *Kiwira Port* limekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kulipa fidia kwa wananchi hao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa kazi iliyofanya lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba ni muda mrefu sana tumeahidiwa kulipwa hizi pesa na sasa hivi ni takribani miaka miwili na wananchi walishasimamisha kazi zao wanazofanya. Ninaomba niulize, je, Serikali sasa itakuwa tayari kufanya marejeo ya thamani ya ardhi na vitu ambavyo vinaenda kuchukuliwa kwa ajili ya kufidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili Wananchi wa Kyela wana hamu sana na hii barabara baada ya kumwondoa yule mkandarasi je, hatua za ujenzi wa barabara hizi zimefikia wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Kyela Kwa mujibu wa sheria tuliyonayo ya fidia muda ukishapita ambao unatakiwa kisheria tutapitia tena uthamini na kupata thamani ya sasa ndiyo wananchi hawa watalipwa lakini kwa thamani ambayo iliyokuwepo ilikuwa ni shilingi bilioni 1,000,762,000 ambazo wananchi walikuwa wanatakiwa walipwe, kwa hiyo tutafanya upya tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara hii ninaomba nimpe habari njema Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kumwondoa yule mkandarasi barabara ile imeshatangazwa na tunategemea tarehe 25 Mwezi huu zabuni zitafunguliwa na kabla ya mwisho wa Disemba mkandarasi atakuwa amepatikana ili aweze kuanza kujenga hiyo barabara, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi wanaopisha barabara ya mchepuo ya Uyole – *Songwe Bypass*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kama tayari tumeshafanya tathmini, wale ambao wako kwenye alama za kijani watalipwa na wale ambao wamewekewa alama nyekundu maana yake hawastahili kulipwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Wizara, tukishafanya tathmini tunawasilisha hayo madai ama hizo fidia Wizara ya Fedha ambapo barabara zote ambazo zimeshawekewa alama taarifa ziko Wizara ya Fedha, wanaendelea kutafuta fedha ili kabla ya kuanza ujenzi wananchi hao walipwe fidia zao, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Sinkamba Kandege.

Na. 151

**Kutangaza Maporomoko ya Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuhakikisha maporomoko ya Kalambo yanatangazwa kitalii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba maporomoko ya maji ya Kalambo yanatangazwa kitalii, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuyaendeleza na kuyatangaza maporomoko hayo, ikiwemo kuboresha miundombinu mbalimbali kwenye hifadhi ya mazingira asilia ya Kalambo, ikiwa ni pamoja na kufanya kampeni za kuyatangaza. Mathalani katika uboreshaji wa miundombinu, Serikali imeboresha barabara, njia za waenda kwa miguu, ngazi za kushuka na kupandisha kwenye maporomoko, miundombinu ya vyoo, mabanda ya kupumzika wageni na eneo la maegesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa matangazo, makala maalumu ziliandaliwa na kurushwa kwenye televisheni, kumekuwa na uandaaji wa matukio na vifurushi vya misimu maalumu, zimefanyika jitihada za kuandaa mabango na vipeperushi na kutumia njia za kidijitali katika kutangaza maporomoko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na jitihada za kuyatangaza maporomoko hayo ili kuvutia watalii wengi kutembelea eneo hilo asilia. Aidha, nitoe rai kwa uongozi wa Mkoa wa Rukwa kuendelea kushirikiana na Wizara katika

kuhamasisha wadau na wawekezaji waliopo katika Mkoa wa Rukwa na nje ya mkoa huo kuwekeza huduma mbalimbali za kijamii, kama vile huduma za malazi kuzunguka maeneo ya maporomoko ya Kalambo kwa lengo la kuwapatia huduma stahiki watalii na wageni wetu wanaotarajiwa kutembelea maporomoko hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutangaza utalii inahitaji uwezeshaji wa kibajeti, je, Serikali itakuwa tayari kuhakikisha kwamba inaiwezesha *TTB* ili iwe na uwezo mkubwa wa kutangaza vivutio vilivyoko Nyanda za Juu Kusini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa tuliwahi kupata ushauri kutoka Serikalini kwamba ili maporomoko ya Kalambo yaweze kufahamika maeneo mengi ni pale ambapo tutakuwa na uwanja mdogo, kwa maana ya *airstrip* na sisi Kalambo tayari tulishatenga eneo hilo. Je, mchakato huo umekwamia wapi ili tuwe na huo uwanja mdogo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kuiwezesha *TTB* kuweza kufanya jukumu lake kubwa la kutangaza vivutio vyetu vya utalii. Kama mtakavyokumbuka katika Bunge la mwaka huu Serikali iliridhia kutenga asilimia sita ya mapato ya utalii yaweze kutumika kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya utalii, hususani kuitangaza sekta hii. Kwa hiyo, nimhakikishie kuwa tupo vizuri kwenye eneo hili na kazi itafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la pili la uwanja wa ndege, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anafahamu, wataalamu wetu wa *TANAPA* walishafanya ziara kwenye eneo hili ambalo wenzetu wa Kalambo walitupa maeneo matatu yanayoweza kujengwa uwanja wa ndege. Tulituma wataalamu wetu na vilevile Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ilifika kule, kuna tathmini inafanyika ndani ya Serikali. Naomba wawe na subira wakati Serikali inajipanga kutekeleza jambo hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Rehema Juma.

Na. 152

**Hitaji la Mabani ya Kukaushia Tumbaku, Ulyankulu**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabani ya kisasa na ya kudumu ya kukaushia tumbaku, Ulyankulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** atajibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, suala la ujenzi wa mabani ni jukumu la kila mkulima wa tumbaku kwa mujibu wa kanuni za kilimo bora cha zao la tumbaku. Hata hivyo, kutokana na upungufu wa mabani uliosababishwa na athari za mvua zilizonyesha msimu wa mwaka 2023/2024 na kusababisha mabani mengi kubomoka, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni mbili katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya ujenzi wa mabani ya kisasa 600.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imepanga kujenga mabani ya kisasa kupitia mpango wa pamoja kati ya wanunuzi na vyama vya msingi kwa kuongeza muda wa mikataba ya

uzalishaji kutoka mkataba wa mwaka mmoja hadi miaka mitatu ambapo pamoja na mambo mengine, mnunuzi atatakiwa kujenga mabani, kwa ajili ya kukaushia tumbaku. Pia wakulima wanahimizwa kujenga mabani ya kisasa au kuboresha mabani ya zamani ili kufikia malengo ya mabani 250,472 yanayohitajika kuongezwa kwa msimu wa mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehema.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kutokana na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuweza kututengea shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kujenga mabani mapya 600 ya kisasa. Ni ukweli kwamba Serikali mmekiri kuna upungufu mkubwa wa haya mabani na kutokana na ukubwa wa tatizo la athari ya mvua ya msimu uliopita mabani haya 600 ni machache sana. Je, sasa Serikali haioni kuna umuhimu wa kutoa ruzuku ili kuweza kuwajengea wakulima wetu wa tumbaku ambao kwa kiasi kikubwa walipata athari kubwa, hali ambayo imesababisha uzalishaji wao kuwa wa kusuasua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kulingana na ukubwa wa athari ya mvua iliyonyesha msimu uliopita, wakulima wengi wa tumbaku wamelowesha mashamba yao, mabani yao yameanguka, na hata mitaji yao kuweza kupotea. Hali hii imesababisha hao wakulima waweze kushindwa kufidia au kulipa madeni kwenye vyama vya msingi. Kutokana na hali hiyo kampuni za ununuzi ziliweka madalali wa kufilisi dhamana na mali za wale wakulima wetu, hali ambayo kampuni hizi za udalali zimesababisha taharuki kubwa sana kwa hao wakulima wetu, wakulima wamenyang'anywa mashamba, nyumba na mali zao nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni sababu na haja kubwa ya kusitisha hawa madalali wa kufilisi wakulima wetu, ilhali hali halisi ya athari ya mvua wameiona? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Rehema kwa kazi nzuri anayoifanya katika jimbo lake, hususani kufuatilia wakulima wa tumbaku. Nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya jitihada ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha athari zote zilizosababishwa na mvua kwa wakulima sisi tunakuwa sehemu na ndiyo maana sehemu ya kwanza tumetenga fedha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kusaidia kujenga mabani ya kisasa, lakini tutaendelea kutenga fedha hata katika mwaka unaokuja, ili kuhakikisha lengo la mabani yote yaliyopo tunaweza kulifikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu tutaendelea kutoa ruzuku katika maeneo mengine ikiwemo mbolea na dawa kwa wakulima wa tumbaku. Vilevile kwenye hili jambo tutaendelea kutenga fedha ili kuhakikisha kwamba tunawasaidia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wale madalali ambao wametumika kunyang'anya mali za wakulima wa tumbaku, niseme sisi kama Wizara, jambo hili tunalifahamu. Tumekuwa tukilifuatilia na tumesema baada ya hapa tutaendelea kufanya vikao zaidi ili kupunguza athari ambazo zimekuwa zikijitokeza kwa wakulima kuuziwa mali zao. Kwa hiyo, tunalifahamu na tunalifanyia kazi, nimuondoe shaka Mheshimiwa Mbunge, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika ambao ni Viongozi wa Ofisi ya Mufti Sheikh Mkuu wa Tanzania kutoka Jijini Dodoma na Dar es Salaam, Dkt. Harith Nkusa, Msemaji Maalum wa Mufti wa Tanzania na Mratibu wa Upandaji Miti Kitaifa na Alhaji Othamn Hotty, Afisa Mipango wa Uhusiano wa Umma Ofisi ya Mufti wa

Tanzania. Hongereni sana kwa kutunza mazingira na kuendelea kupanda miti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Waheshimiwa Wabunge; yupo mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na huyu ni rafiki yake ambaye ni mfanyabiashara kutoka *Washington DC*, nchini Marekani, karibu. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa ambaye ni mpiga kura wake kutoka Igunga, anaishi Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Eric Shigongo ambaye ni mpiga kura wake kutoka Buchosa, Mkoa Mwanza. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, mpiga kura wake kutoka Tarime Vijijini, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Deo Sanga ambaye ni mjukuu wake kutoka Makambako, Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga na hawa ni wadogo zake kutoka Mbogwe, Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mwenyekiti na Katibu Kata ya Maghunga kutoka Jimbo la Singida Kaskazini. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa ambao ni watoto wake kutoka Mjini Zanzibar. *(Makofi)*

Vilevile wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Ghati Chomete, makada wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Tarime, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Omar Ali Omar na hawa ni walimu wa Madrasa kutoka Jimbo la Wete, Kaskazini Pemba. *(Makofi)*

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo ambao ni washiriki wa Kanisa la *Destiny City Church* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula na hii ni Kwaya ya Mtakatifu Maria De Mathias, Parokia Bikira Maria, Mama wa Damu Azizi ya Yesu kutoka Kisasa, Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 57 wa Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, hawa ni kutoka Taasisi ya Bega kwa Bega na Mama Samia na Tanzania kutoka Mkoa wa Tanga, Pwani na Singida. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo; yupo Mwinjilisti wa Kanisa la *Evangelist Assemblies of God Tanzania* kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Ndugu Maimuna Mnyika na Ndugu Salima Kizua ambao ni wajasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Muswada huu naupeleka kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2024 *(The Environmental Management (Amendment) Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naelekeza Muswada huu uende katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *(The Labour Laws (Amendments) Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naelekeza Muswada huu uende Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa Mwaka 2024**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naelekeza Muswada huu uende Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, Mitaji ya Umma.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge, sasa zimemalizika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja ya Kuahirisha Bunge. Sasa namuita Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa rehema zake zilizotufikisha katika siku ya leo mahsusi kwa ajili ya kuhitimisha shughuli za Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kutambua kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza Bunge kwa weledi mkubwa. Sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakubaliana nami kwamba viwango vya umahiri vya Mheshimiwa Spika vimeendelea kuongezeka. Kwa kila Mkutano tumeendelea kushuhudia hekima kubwa ambayo imefanya vikao vyote kumalizika kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninatambua mchango wako wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge ambao ni Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika katika kuliongoza Bunge letu tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapohitimisha Mkutano huu wa Kumi na Saba wa Bunge la Kumi na Mbili tunafahamu kuwa wewe pamoja na wasaidizi wako mmekuwa chachu ya mafanikio ya Mkutano huu. Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu tunawashukuru sana na tunamwomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa nguvu na hekima ya kulitumikia Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kazi kubwa waliyoifanya katika Mkutano huu. Serikali kupitia Waheshimiwa Mawaziri tumepokea maoni, ushauri na hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge. Nikiri kwamba wakati wote michango ya Waheshimiwa Wabunge katika mijadala mbalimbali imekuwa na tija sana kwetu Serikali. Nitumie nafasi hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imepokea michango yote na itaifanyia kazi kwa mustakabali wa maendeleo ya wananchi wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe salamu za pole; tangu kuahirishwa kwa Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge la Kumi na Mbili yapo majanga yaliyotokea hapa nchini na kusababisha athari mbalimbali kwa Watanzania wenzetu. Nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Watanzania wote waliopatwa na majanga hayo au waliopoteza wapendwa wao na uharibifu wa mali. Kwa wale waliojeruhiwa ninamwomba Mwenyezi Mungu awape uponyaji wa haraka, Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 29 Oktoba, 2024 tulipokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Jenerali David Bugozi Musuguri, aliyewahi kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania. Ninatoa pole hizi kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa msiba huo wa Jenerali Musuguri. Jenerali Musuguri atakumbukwa

kwa ujasiri wake na utumishi uliotukuka katika Jeshi la Wananchi na hasa aliposhiriki kikamilifu kwenye vita ya Uganda ambayo tuliibuka kuwa washindi, yeye akiwa Jenerali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tarehe 2 Novemba, 2024 tuliondokewa na Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Mheshimiwa Kipenka Msemembo Musa aliyewahi kutumikia kwa nyakati tofauti mihimili yote ya dola. Kama mtakumbuka Mheshimwa Kipenka aliwahi kulitumikia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nafasi ya Katibu wa Bunge kuanzia mwaka 2000 hadi 2004. Ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote. Mheshimiwa Kipenka atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa kwa nafasi zote alizozitumikia wakati wa uhai wake. Bwana ametoa, Bwana ametwaa jina la bwana lihimidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitoe salamu za pongezi; kama mtakumbuka tarehe 16 Septemba, 2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa viongozi. Mheshimiwa Rais alimteua Ndugu Baraka Ildephonce Leonard kuwa Katibu wa Bunge letu na Ndugu Nenelwa Mwihambi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Ndugu Baraka Ildephonce Leonard kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu wetu wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nimhakikishie kuwa Serikali itampa ushirikiano wote unaohitajika wakati wote anapotekeleza majukumu yake ili aweze kutekeleza vizuri majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza pia Mheshimiwa Jaji Nenelwa Mwihambi, kwa uteuzi huo na nimtakie utekelezaji mwema wa majukumu yake mapya. Vilevile nimshukuru kwa kazi nzuri aliyoifanya wakati wote akiwa Katibu wa Bunge hapa na tunamtakia kazi njema kwenye Mahakama alikopelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nampongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, kwa kuongoza Mkutano wa 149 wa Umoja wa Mabunge Duniani uliofanyika kuanzia tarehe 13 Oktoba, 2024 huko Geneva, Uswisi. Mkutano huo ulikuwa na lengo la kujadili kwa mapana kuhusu masuala yanayoathiri amani ya dunia, mazingira, haki za binadamu na demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tuna kila sababu ya kujivunia ushupavu aliouonesha wakati wa mkutano huo na jinsi alivyoonesha msimamo usioyumba wakati wote. Sina shaka, uongozi wake utaweka alama katika historia ya uongozi wa Umoja wa Mabunge Duniani, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla, tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Spika ili aendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Sote kwa pamoja tumuombe Mwenyezi Mungu azidi kumpa uzima, hekima na nguvu katika kuutumikia Umoja wa Mabunge Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shughuli za Bunge; Mkutano huu wa Kumi na Saba wa Bunge la Kumi na Mbili ulipokea na kujadili taarifa mbalimbali kutoka kwa Kamati za Kudumu za Bunge, maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na majibu ya Serikali sambamba na kujadili na kupitisha Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge waliuliza maswali 133 ya msingi na mengine 491 ya nyongeza ambayo yalijibiwa na Serikali. Halikadhalika, maswali sita ya papo kwa papo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Bunge hili Serikali imewasilisha miswada minne ambayo ililetwa na kusomwa kwa mara ya kwanza. Miswada iliyowasilishwa ni kama ifuatayo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment of 2024);*

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024 *(The Environmental Management (Amendment) Act, 2024);*

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 *(The Labour Laws (Amendments) Act, 2024);* na

(iv) Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi wa Mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji iliwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026. Mpango huo umejikita katika kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo ya maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliwasilisha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ikumbukwe kwamba Mpango huo uliopitishwa na Bunge lako, ndiyo wa mwisho ambao unaenda kuhitimisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao katika Mpango huu pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kwa mwaka 2025/2026. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaweka mkazo katika maeneo ya miradi ya kielelezo yenye manufaa na matokeo makubwa na kujielekeza katika vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026. Vipaumbele hivyo ni:-

(i) Kuchochea uchumi shindani na shirikishi;

(ii) Kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa bidhaa viwandani na utoaji huduma;

(iii) Kukuza uwekezaji na biashara;

(iv) Kuchochea maendeleo ya watu; na

(v) Kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu ninukuu maneno ya mwanatasnia ya filamu na muziki kutoka Marekani, Ndugu Deborah K. Allen aliyesema (kwa tafsiri isiyo rasmi); "Hata kama una bajeti kubwa kiasi gani, huwezi kufanya kila jambo." Maana yake ni kwamba ni muhimu kuweka kipaumbele kwa masuala ya msingi ambayo yatakuwezesha kufikia ndoto zako, bila kujali kiasi gani cha fedha ulichonacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa rai kwa watendaji wote Serikalini kuhakikisha kwamba vipaumbele vilivyoanishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026 vinatafsiriwa vema kwenye mipango ya taasisi zao ili kwa pamoja tuweze kufikia mwisho mwema wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifanye mapitio ya Taarifa ya Kamati za *PAC* na *LAAC* kuhusu hesabu zilizokaguliwa na *CAG* kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Taarifa ya Kamati ya *PIC* kuhusu Uwekezaji na Mitaji ya Umma kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano huu wa Kumi na Saba wa Bunge lako umepokea na kujadili kwa kina Taarifa za Kamati za Bunge ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC),* Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizi za Kamati zinazotokana na Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ninalipongeza Bunge lako Tukufu kwa kuchambua kwa kina hoja zote za ukaguzi zinazohusu matumizi ya fedha za umma pamoja na kutoa maazimio ambayo kimsingi ni maelekezo mahsusi kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi kwamba Serikali imeendelea kufanyia kazi mapendekezo yanayotolewa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi chini ya uongozi wa Ndugu Charles E. Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Vilevile Serikali imeendelea kuzingatia maelekezo yote yanayotolewa na Bunge lako Tukufu kupitia maazimio na hoja zilizotolewa. Lengo la Serikali ni kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika kusimamia na kudhibiti ipasavyo ukusanyaji wa mapato na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zote zimeainishwa kwa ajili ya utekelezaji, hivyo basi, ninaziagiza Wizara zote kuandaa kwa wakati taarifa za utekelezaji wa maazimio yote kulingana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge na kuziwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu ili iweze kuwasilisha taarifa ya Serikali kwa Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuwakumbusha Maafisa Masuuli na watendaji wote Serikalini kuhakikisha kuwa wanazingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha za umma ili kutimiza ndoto na malengo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwaletea Watanzania maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha robo ya mwaka 2024/2025; Serikali imeendelea kusimamia makusanyo katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/2025 ambapo jumla ya shilingi trilioni 11.55 zimekusanywa kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 7.93 ni mapato ya ndani, sawa na 99.4% ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 7.97. Mapato hayo yanajumuisha mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato

Tanzania shilingi trilioni 7.09, mapato yasiyo ya kodi yaliyokusanywa na Wizara na Idara zinazojitegemea shilingi bilioni 518.32 na mapato kutoka vyanzo vya Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi bilioni 321.32.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio hayo yanatokana na mikakati mbalimbali iliyowekwa na Serikali, mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kuimarisha na kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato na kuhamasisha matumizi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania inayoongozwa na Ndugu Mwenda na Taasisi zote zinazohusika katika ukusanyaji wa mapato kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha, niwapongeze wananchi wote kwa kujitoa kwa dhati na kuhakikisha kuwa wanalipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Vilevile wafanyabiashara wanapaswa kutoa risiti na wananchi kuhakikisha wanadai risiti kila wanapofanya manunuzi ya bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe watendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kuendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato na utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa ulipaji wa kodi kwa manufaa ya nchi yetu. Kwa upande mwingine, ninazikumbusha halmashauri zote nchini kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza wigo wa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha robo ya kwanza ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025, ridhaa ya shilingi trilioni 11.67 ilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha mishahara, kugharimia Deni la Serikali na matumizi mengineyo. Matumizi ya maendeleo yamejumuisha kugharimia miradi na programu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa *(SGR)*, ujenzi na ukarabati wa barabara, madaraja na viwanja vya ndege, Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere, miradi ya

umwagiliaji, kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania na mradi wa usambazaji umeme vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mengine ni kuwezesha mpango wa elimu bila ada, mitihani ya darasa la saba pamoja na kidato cha nne, maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024, uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura na maandalizi ya mashindano ya kuwania Kombe la Mataifa ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie masuala ya utabiri wa hali ya hewa kwa sasa hapa nchini. Mabadiliko ya tabianchi yamekuwa na athari ambazo tumekuwa tukizishuhudia. Msimu uliopita nchi yetu iliathiriwa na vimbunga na mvua za *El-Nino*. Kutokana na athari hizo, Serikali imechukua hatua muhimu za kurejesha hali kwa kukarabati miundombinu ya barabara, madaraja na makalavati yaliyoharibiwa. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa kuridhia matumizi ya fedha shilingi bilioni 130 kwa ajili ya kurejesha miundombinu hiyo kwa dharura ambapo kazi zilifanyika usiku na mchana. Vilevile kutumika fedha shilingi bilioni 868.56 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kudumu ili kuhakikisha mawasiliano yanarejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu huu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ilitoa utabiri wa mwelekeo wa msimu wa mvua za vuli kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Desemba, 2024 na mwelekeo wa mvua za msimu zinazoanza Novemba, 2024 hadi Aprili, 2025. Kutokana na utabiri huo, msimu wa mvua za vuli unatarajiwa kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia hapa ili Watanzania waelewe kwamba msimu wa mvua za vuli unatarajiwa kutawaliwa na vipindi virefu vya ukame na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini inaonesha mvua za msimu zitakuwa za wastani hadi chini ya wastani na zinatarajiwa

katika maeneo ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Songwe, Singida, Dodoma, Kaskazini na Mashariki mwa Mkoa wa Lindi na Kaskazini mwa mikoa ya Mbeya na Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika Mikoa ya Njombe, Ruvuma, Mtwara, maeneo ya Kusini na Magharibi mwa Mkoa wa Lindi, Kusini mwa Mikoa ya Mbeya, Iringa na Morogoro. Mvua nyingi zinatarajiwa katika kipindi cha nusu ya pili ya msimu ambacho ni mwezi Februari hadi Aprili, 2025 ikilinganishwa na nusu ya kwanza ambacho ni Novemba, 2024 hadi Januari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, upo uwezekano wa kujitokeza vipindi vifupi vya mvua kubwa ambapo pia kunaweza kuwa na mafuriko, upepo mkali na ongezeko la joto. Hali hiyo inaweza ikasababisha athari mbalimbali ikiwemo uharibifu wa miundombinu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe watulivu, Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya Bunge ili tusikilize taarifa ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuzielekeza Kamati za Maafa katika ngazi ya Kijiji, Wilaya, Mkoa na Taifa kujipanga kikamilifu kukabiliana na changamoto za mvua endapo zitajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa wakulima wote kutumia mvua hizo kulima mazao yanayoendana na upatikanaji wa mvua katika maeneo yao na kuzingatia ushauri wa wataalamu wa kilimo. Kwa upande mwingine, Watanzania wote tuendelee kujenga tabia ya kufuatilia taarifa za utabiri wa hali ya hewa pamoja na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Serikali ikiwemo kuhama kwenye maeneo hatarishi na kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo yaliyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo tukielekea kwenye kilimo, naomba kutoa taarifa ya uratibu na upatikanaji wa

pembejeo. Kwa kuwa tunaelekea katika msimu wa kilimo, ninaelekeza mikoa na halmashauri kuhamasisha wakulima kujisajili kwenye daftari la mkulima na kuwapatia namba za usajili. Pia waendelee kuwahamasisha wauzaji wa pembejeo za kilimo kujisajili katika mfumo wa kidigitali ili waweze kuuza mbolea na mbegu bora za mahindi kwa wakulima kupitia utaratibu wa ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mnaporejea kwenye majimbo yenu endeleeni kuwahimiza wakulima wote wa zao la mahindi ambao hawajajisajili ili wajisajili kwenye daftari la mkulima. Daftari hilo linapatikana katika Ofisi za Vijiji/Mitaa na wakulima watakaojisajili watapata namba maalumu ya mkulima watakayoitumia kununulia mbolea na mbegu bora za mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie sekta ya elimu na hasa usimamizi wa elimu msingi. Ni kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuanza shule wanaandikishwa na kumaliza mzunguko wao wa masomo kwa mujibu wa ngazi husika, lengo likiwa ni kuhakikisha tunajenga jamii ya Watanzania walioelimika, wenye maarifa, stadi na mtazamo chanya utakaowezesha kuchangia katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa inaendelea na maandalizi ya uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali na darasa la kwanza kwa kutumia maoteo yanayotokana na takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Hapa matarajio ni kuandikisha watoto wa elimu ya awali zaidi ya milioni 1.8 na wanafunzi wa darasa la kwanza wapatao milioni 1.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la uandikishaji limekwishaanza na ninatoa wito kwa wazazi na walezi kuhakikisha kwamba wanawafikisha kwa watendaji wetu wa vijiji ili kuhakikisha wanawaandikisha watoto wote wenye umri wa kuanza shule wakiwemo watoto wenye mahitaji maalumu.

Naelekeza Wakurugenzi wa Halmshauri zote kuwapangia majukumu Watendaji wa Vijiji na Kata ili kuhamasisha wazazi na walezi kwenye maeneo yao, pamoja na makundi mbalimbali ya kijamii ili yaweze kutoa elimu kwa wazazi na walezi juu ya umuhimu wa kwenda kumwandikisha mtoto kuanza masomo kwenye ngazi ya awali na darasa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunaratajia kupokea wanafunzi watakaoanza kidato cha kwanza kuanzia mwezi Januari, 2025. Ili kuhakikisha wanafunzi hao wanaanza masomo kwa wakati mmoja, ninaelekeza viongozi wa Mikoa na Wakurungezi wa Halmashauri zote kusimamia kikamilifu ujenzi wa miundombinu inayotosha kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi hao ifikapo mwezi Januari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya utoaji wa mikopo ya elimu ya juu; Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa fursa za masomo ya elimu ya juu pamoja na taaluma za kipaumbele kwenye vyuo vya kati, imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kutoa mikopo ya wanafunzi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 787.4 kwa ajili ya wanafunzi 245,799 ambapo hadi sasa jumla ya shilingi bilioni 600.6 zimetolewa kwa wanafunzi 189,641.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuendelea kuongeza fedha za kukopesha wanafunzi, kumekuwa na ongezeko la wahitaji wa mikopo hiyo. Ili kukabiliana na changamoto hii Serikali inaangalia uwezekano wa kuishirikisha sekta binafsi katika ugharimiaji wa elimu ya kati na ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maandalizi ya Uchaguzi wa Viongozi wa Serikali za Mitaa, uandikishaji na maandalizi ya orodha ya wapigakura wa Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni takwa la Kanuni za Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa za mwaka 2024. Kanuni hizo zinaelekeza kuwa kutakuwa na orodha ya wapigakura ambayo itatumika katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Mtaa, Mwenyekiti wa Kitongoji na Wajumbe wa Serikali za Vijiji na Kamati za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza wananchi wote waliojitokeza kwa wingi wakati wa uandikishaji. Vilevile nitoe rai kwa wananchi wote kama walivyojitokeza kwenye kujiandikisha, vivyo hivyo wajitokeze siku ya Jumatano, tarehe 27 Novemba, 2024 ili kupiga kura kwa kiongozi wanayeona anaweza kuwaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitoe maelezo mahususi juu ya nishati safi ya kupikia. Kama mnavyofahamu kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Katika Mkutano wa 79 wa Baraza la Umoja wa Mataifa uliofanyika Septemba, 2024, Mheshimiwa Rais alipongezwa kwa kuwa kinara katika kuhakikisha malengo ya kuhamia kwenda nishati safi ya kupikia yanatimia ifikapo mwaka 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umahiri wa Mheshimiwa Rais, Tanzania imeombwa na kukubali kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Nishati Afrika utakaofanyika tarehe 27 hadi 28 Januari, 2025. Lengo la mkutano huo ni kuhamasisha ushirikiano mpana wa kufikisha nishati ya umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika ifikapo mwaka 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Novemba 6, 2024 niliamua kutembelea Taasisi zetu zikiwemo Kambi ya JKT Makutupora, Shule ya Sekondari ya Wasichana, Msalato na Gereza la Isanga kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhusu matumizi ya nishati safi na salama. Mambo niliyoyabaini ni haya yafuatayo:

(i) Kambi ya JKT Makutupora na makambi yote ya JKT yametekeleza kwa kujenga mifumo ya gesi kwa kushirikiana na Kampuni ya Taifa *Gas*. Pia kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* wanatekeleza mradi utakaowapatia majiko banifu na sufuria zake 291 kwa vikosi vyote vya JKT, majiko ya gesi na sufuria zake 180, mitambo ya *biogas* tisa na majiko yake, mashine za kutengeneza mkaa mbadala 60

ambapo mafunzo kwa vijana kuhusu mitambo hiyo yataendeshwa na *REA*.

(ii) Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato imetekeleza maelekezo hayo kwa kujenga mifumo inayotumia mkaa mbadala ujulikanao kama KUNIPOA ambao unatengenezwa kwa kutumia maganda ya miwa na takataka za miti ambao umewasaidia kupunguza gharama za uendeshaji eneo la jikoni kuliko ilivyokuwa awali. Nilielezwa kwamba zamani walikuwa wakitumia shilingi milioni 4.5 kila mwezi kununua kuni za kawaida, lakini kwa sasa wanatumia shilingi milioni 1.3 kwa kutumia KUNIPOA ambazo zinaendelea kutekeleza mapishi kwenye jiko lao.

(iii) Gereza Kuu la Isanga chini ya Jeshi la Magereza limeanza kutumia majiko banifu kwa kutumia mkaa rafiki unaotengenezwa na *STAMICO*. Jeshi hilo linaendelea kutekeleza mpango wa matumizi ya nishati safi ya kupikia chakula cha wafungwa na mahabusu gerezani ambao utahusisha vituo 211 yakiwemo magereza 129, Ofisi 26 za Magereza za Mikoa na Vyuo vya Magereza vinne, Makao Makuu, Bohari Kuu, Hospitali kuu ya Jeshi, Karakana, Shule ya Sekondari Bwawani, Kikosi Maalum na Kambi za Magereza 47.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuweka msisitizo wa matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kwa msingi huo nielekeze masuala yafuatayo:-

(i) Taasisi zote zenye kuandaa chakula cha watu zaidi ya 100 zihakikishe zinatekeleza maagizo haya ya kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia;

(ii) Wizara ya Nishati iendelee kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia;

(iii) Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kote nchini, wafanye ukaguzi kwenye taasisi zilizomo katika maeneo yao mathalan majeshi, polisi, vyuo vya elimu ya kati na ya juu, vyuo vya Wizara mbalimbali kama elimu, afya na kilimo ili maeneo yanayopaswa kubadilisha mifumo yao ya nishati ya kupikia kwa vile yana idadi kubwa ya walaji wa vyakula. Aidha, wajasiriamali wanaopika chakula cha watu wengi kama vile kwenye harusi na maeneo mengine wahamasishwe ili nao wabadilishe teknolojia zao ili ziendane na matumizi ya nishati safi ya kupikia.

(iv) Ninawaelekeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wote ifikapo Desemba, mwaka huu watoe taarifa ya utekelezaji kuonesha ni taasisi ngapi tayari zimetekeleza agizo hilo, hii ni kwa taasisi zote za umma na binafsi. Lengo ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2033 80% ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia ambayo ni: Gesi, umeme, makaa ya mawe, KUNIPOA zinazotokana na utengenezaji wa wajasiriamali kupitia takataka.

(v) Wananchi wa Tanzania tuendelee kubadili mfumo wa maisha hususan taratibu za kupika kwa kutumia nishati safi wakati wa kuandaa chakula ili kuachana na nishati chafu ya kupikia inayohusisha kuni na mkaa unaotokana na miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie michezo kuwa eneo la mwisho. Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa Sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo imeendelea kuleta tija na mafanikio makubwa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati inayofanywa na Serikali imekuwa chachu ya mafanikio tunayoendelea kuyashuhudia katika Sekta ya Michezo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kutenga fedha katika bajeti ya kila mwaka ili kufanikisha mipango ya maendeleo ya Sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Sekta ya Michezo imeongezeka kufika shilingi bilioni 285.31 katika mwaka wa fedha 2024/2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 54.74 katika mwaka wa fedha 2021/2022. Ongezeko hilo ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja na huduma saidizi kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya *AFCON* 2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maandalizi ya *AFCON* 2027. Kama Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka, Serikali imeshaanza mchakato wa maandalizi ya mashindano ya *AFCON* yanayotarajia kufanyika mwaka 2027. Hatua za maandalizi zinatekelezwa kwa kuzingatia mpango mkakati wa utekelezaji wa maandalizi ya mashindano ya *AFCON* 2027. Miongoni mwa masuala yanayotekelezwa katika mpango huo ni pamoja na: ujenzi na ukarabati wa miundombinu, uendelezaji wa masoko ya utalii, uandaaji wa timu ya Taifa, ulinzi na usalama pamoja na mpango wa matangazo na hamasa kwa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miundombinu, Serikali inatekeleza miradi ya ujenzi wa viwanja vya michezo ikiwemo kiwanja cha Arusha. Vilevile, inakarabati viwanja vya Benjamin Mkapa, Uhuru na Amani - Zanzibar ili kukidhi vigezo vya mashindano ya *CHAN* yanayotarajiwa kufanyika Februari, 2025 na *AFCON 2027*. Aidha, Serikali inaendelea na ukarabati wa viwanja mbalimbali vya mazoezi vitakavyotumika katika mashindano hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa wanamichezo wote walioshiriki katika mashindano mbalimbali kitaifa na kimataifa na kulileteea Taifa letu heshima kubwa. Kama wahenga walivyosema; "asiyekubali kushindwa si mshindani," nitoe rai kwa wanamichezo ambao hawakufanikiwa kupata ushindi wajipange upya kwa ajili ya kushiriki katika mashindano mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kutoa pongezi zangu kwa mshindi wa mchezo wa ngumi, mwanamasumbwi Abdul Ramadhan Ubaya ambaye katika pambano la *light heavy weight* lililofanyika tarehe 25 Oktoba, 2024 nchini Urusi alifanikiwa

kumshinda kwa *knock out* bondia Ibragim Estemirov kutoka Urusi. Vilevile nitumie nafasi hii kuwapongeza mabondia wengine ambao wamekuwa wakifanya vizuri katika mashindano mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninaipongeza Timu ya Taifa ya Wanaume ya Mchezo wa Kriketi kwa kufuzu mzunguko wa pili wa Mashindano ya Wanaume ya *ICC* Ukanda wa Jangwa la Sahara yatakayofanyika Machi, 2025. Ninawapongeza sana kwa ushindi huo na kuwatakia kila la kheri katika hatua inayofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kushuhudia wachezaji wa mpira wa miguu wakifanya vizuri katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi. Nianze kwa kuwapongeza Timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 12 kwa kufanikiwa kutinga katika nusu fainali ya mashindano ya *Female Universal Youth Cup* yaliyofanyika Dingnan, nchini China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza pia, Timu ya Taifa ya Wavulana chini ya miaka 16 kwa kushika nafasi ya pili katika mashindano ya *FIBA* Kanda ya tano Afrika yaliyofanyika hivi karibuni. Wakati huo huo, Timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 20 (*Ngorongoro Heroes*) imetwaa kombe la *CECAFA* baada ya kuishinda timu ya Rwanda mabao matatu kwa moja. Vilevile, katika mashindano ya nusu fainali yaliyofanyika tarehe 18 Oktoba, 2024 uwanja wa *KMC* jijini Dar es Salaam na kufuzu *AFCON* 2027 baada ya kuifunga Timu ya Kenya chini ya miaka 20 mabao mawili kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Ushiriki wa Vilabu vyetu kwenye Mashindano ya Kimataifa. Vilabu vya Tanzania vimeendelea kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa, ambapo kwa msimu wa mwaka 2023/2024 Tanzania ilifanikiwa kuingiza timu nne. Katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika timu mbili za Azam na Yanga na katika Kombe la Shirikisho timu mbili za Simba na *Coastal Union.* Aidha, Timu za Yanga na Simba zimefanikiwa kuingia hatua ya makundi katika mashindano ya Klabu Bingwa na Shirikisho. Ninazipongeza na tunawatakia

mafanikio mema na huku timu za ligi kuu ya Tanzania tunashuhudia zikiendelea vizuri kupambana na tunawatakia kila la kheri kwenye mashindano yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Spika, na zaidi ya yote kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuchangia mjadala wa Bunge hili kwa kuzingatia manufaa makubwa ya ustawi wa Taifa letu. Kama mnavyofahamu uwepo wa Bunge hili ulikuwa ni muhimu ili kuweza kupata maoni na ushauri kutokana na hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninamshukuru Katibu wa Bunge, wasaidizi wake na watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri walizotupatia kwa kipindi chote tulichokuwa tukitekeleza majukumu yetu ya Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge la Kumi na Mbili. Pia ninawashukuru viongozi na watendaji wa Serikali na Taasisi zake kwa kuendelea kufanyia kazi masuala mbalimbali ambayo yamekuwa yakiwezesha uwasilishaji wa hoja zilizotokana na mijadala ya Bunge. Ninavishukuru pia vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kuhakikisha kwamba mikutano ya Bunge inaendelea kufanyika katika hali ya utulivu na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, ninawashukuru wanahabari kwa kufanya uchambuzi mzuri wa hoja na mwenendo mzima wa Bunge letu na pia kwa kuwahabarisha wananchi. Kadhalika, ninawashukuru madereva waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la michezo nimeshasema nimetakia timu zote za ligi kuu ziendelee vizuri na kweli leo nimetumia nafasi hii kuzipongeza tu timu za ligi kuu na hatua walizofikia na tunawatakia kila la kheri kwa mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunaelekea mwishoni mwa mwaka na hatutakuwa na mkutano mwingine ndani ya mwaka 2024, nitumie nafasi hii kuwatakia Waheshimiwa Wabunge

wote, Watanzania wote na waumini wote wa Kikristo, sherehe njema ya sikukuu ya Krismasi na heri ya mwaka mpya wa 2025. Niwatakie safari njema Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnaporejea majimboni kwenu na Mwenyezi Mungu awafikishe salama kwenye vituo vyenu vya kazi na tuwatakie kila la kheri na mpate mafanikio makubwa kwenye majimbo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kama ambavyo nimemaliza sihitaji kuongeza kitu kingine chochote mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya maelezo hayo, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 28 Januari, 2025 siku ya Jumanne, saa tatu kamili asubuhi katika ukumbi huu hapa jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, ninaomba kutoa hoja, ahsante *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono na Bunge Zima. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa weledi wako, uwezo wako na utiifu wako kwa Taifa hili; hongera sana. *(Makofi)*

Sasa nitawahoji, wanaoafiki Bunge liahirishwe mpaka tarehe 28 Januari, 2025 waseme ndiyo. Wasioafiki waseme siyo.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Wale ambao hawakuafiki nawapa maelekezo waisubiri timu ya Tabora kuipokea hapa. Walioafiki wameshinda. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge kuwa Ofisi ya Bunge imeandaa Jarida la Bunge Tolea la Nane. Jarida hilo pamoja na mambo mengine linaelezea masuala mbalimbali ya kibunge ikiwemo matukio yaliyojiri katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge. Jarida hilo tayari limeshawekwa kwenye vishikwambi vyenu naomba mvifungue na msome.

Katibu wa Bunge anaomba kuwakumbusha Wabunge wote kuwa fomu za maadili ziko *online* na mwisho wa kujaza ni tarehe 30 Desemba. Kama usipotimiza sharti hili la kikatiba jihesabu tarehe moja Januari wewe siyo Mbunge. Ndiyo Katiba na sheria zinavyosema hivyo. Kwa hiyo, nawaomba muanze kuzijaza kuanzia leo ziko *online* na ziko vizuri tu mtaweza kuzielewa.

Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri mliyofanya. Serikali jana imetoa darasa zuri sana, haya nendeni mkayaseme majimboni kuhakikisha Chaguzi za Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji vyote tunashinda Chama Tawala cha CCM. Niwatakie kila la kheri kurudi nyumbani. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**NAIBU SPIKA:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe 28 Januari, 2025.

*(Saa 5.18 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 28 Januari, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*